

Ofisi za Idara:

1700 - 155 Carlton St.
Winnipeg MB R3C 3H8
Nambari ya simu.
204- 945-2476
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-782-8403
Nambari ya kutuma Faxi:
204-945-6273
Anwani ya mtandao:
rtb@gov.mb.ca

143-340 9th Street
Brandon MB R7A 6C2
Nambari ya simu.
204-726-6230
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-656-8481
Nambari ya kutuma Faxi:
204-726-6589
Anwani ya mtandao:
rtbbrandon@gov.mb.ca

113-59 Elizabeth Dr.
Thompson MB R8N 1X4
Nambari ya simu.
204-677-6496
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-229-0639
Nambari ya kutuma Faxi:
204-677-6415
Anwani ya mtandao:
rtbthompson@gov.mb.ca

The Residential Tenancies Branch Idara ya Kupangisha Makaazi

MAMBO MAALUM

Kuongeza Kodi ya Nyumba

Mara nyingi, mpangishaji anaweza kuongeza kodi ya nyumba baada ya miezi 12. Kila mwaka, serikali hupeana kikomo cha kodi itakayoongezwa. Hiki kikomo huitwa taratibu za kuongeza kodi. Ukitaka kujua mengi kuhusu taratibu za kodi zilizopo sasa na zilizokuwako awali, tembelea idara ya kupangisha makaazi kwa mtandao wa intaneti www.manitoba.ca/rtb.

Je, Mpangishaji Anaweza Kuongeza kodi vipi?

Kabla ya kuongeza kodi, lazima mpangishaji apeeane mpangaji ilani ya miezi 3. Ilani hii lazima:

- Iwe kwa maandishi
- Ionyeshe kiasi cha kodi cha sasa
- Ionyeshe ni pesa ngapi itaongezwa, kwa hela za dola na pia kwa asilimia (Kwa mfano hii ni nyongesa ya \$15.00 au 3%);
- Ieleze ni kiasi kigani ambacho mpangishaji anaruhusiwa kuongeza
- Ieleze ni lini kodi iliyoongezwa itakopoanzishwa
- Ieleze kwamba kuongeza kodi si halali hadi mpangaji apewe ilani ya miezi 3
- Ionyeshe taratibu ya kuongeza kodi kila mwaka, kwa mfano 1.5%
- Ieleze kwamba mpangaji ana uhuru wa kutokubaliana na kiasi cha kodi inayoongezwa

Mpangishaji anadaiwa vile vile kupeana Idara ya Kupangisha Makaazi ilani iliyoandikwa kuhusu kuongeza kodi katika mda wa siku 14 baada ya kufahamisha mpangaji.

Je Mpangaji anaweza kufanya nini?

Ikiwa mpangaji hakubaliani na kiasi cha kodi iliyoongezwa, anaweza kuandika barua kwa Idara ya Kupangisha Makaazi akieleza kwa nini hakubaliani. Barua hii ni lazima ifike kwenye idara hiyo siku 60 kabala ya kuanza kwa kodi iliyoongezwa.

Kodi inayozidi kanuni iliyowekwa na Idara ya Kupangisha Makaazi

Wapangishaji wanaotaka kuongeza kodi zaidi ya kanuni iliyowekwa, lazima wapate kibali kutoka kwa Idara ya Kupangisha Makaazi. Lazima mpangishaji aombe ruhusa kwa kuandika barua kwa idara. Lazima waombe ruhusa hii katika muda wa siku 14 baada ya kupeana ilani kwa mpangaji.

Wapangaji wanaweza kuona na kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo ya kuongeza kodi kutoka kwa mpangishaji. Mpangishaji anaweza kuona na kutoa maoni yake kuhusu maelezo yaliyopeanwa na wapangaji. Idara ya Kupangisha Makaazi itaamua kiasi cha kodi itakayoongezwa. Uamuzi huu utajumuisha vyumba vyote kwenye mjengo au jumuiya za nyumba zilizohusika.

(pindua ukurasa)

Kupinga Uamuzi

Ikiwa mpangishaji au mpangaji hakubaliani na uamuzi wa idara kuhusu kuongeza kodi, ana haki ya kutia rufani kwenye Tume ya Kupangisha Makaazi kwa anuani 1650 – 155 Carlton Street, Winnipeg MB R3C 3H8, katika mda wa siku 14 baada ya kupokea uamuzi wa Idara ya Kupangisha Makaazi.

Tume itateua jopo itakayotazama rufani. Mwakilishi wa serikali, mwakilishi wa mpangishaji na mwakilishi wa mpangaji wataunda jopo hii. Jopo itapanga mkutano au kusikiliza kwa kesi. Kila mhusika ataelezwa awali. Baada ya kusikia kesi, Tume itaamua. Uamuzi wa Tume ni wa mwisho.

Je, Sheria ya kuongeza kodi inahusu kila mpangaji?

Sheria hizi huhusisha makao ya kukodisha mbali mbali kama nyumba iliyosimama peke, au nyumba zilizounganishwa mbili, au chumba katika nyumba, au jengo la orofa.

Kanuni ya kuongeza kodi haihusu vyumba vifwatavyo:

- Nyumba mpya; ikiwa makaazi yalijengwa na kukaliwa baada ya tarehe ya Aprili 9, 2001, kodi ya vyumba hivi haitaongezwa kwa mda wa miaka 15; Ikiwa makaazi yalijengwa na kukaliwa baada ya tarehe ya Mechi 7, 2005, kodi haitaongezwa kwa mda wa miaka 20.
- Vyumba vinavyokodesha kwa zaidi ya pesa kiasi fulani; kiasi hiki kinaweza kubadilika kila mwaka; angalia kwenye mtandao Idara wa intaneti hapa www.manitoba.ca/rtb ili upate maelezo kamili au upige simu au uandike barua kwa idara ili upokee ujumbe kamili
- Vyumba ambavyo vinachungwa na, ama vinachungwa kwa niaba ya Serikali ya Canada, Serikali ya Manitoba au manisipaa
- Vyumba vya mwajiriwa au mwenye kuchunga jengo
- Vyumba ambavyo vimepangishwa kwa maisha ambavyo vimekodesha na ofisi zisizo za faida

Hata kama kanuni hizi hazizingatiwi, mpangishaji anahitajika kupeana ilani ya mda wa miezi 3 kwa maandishi ikiwa anataka kuongeza kodi.

Kwa maelezo zaidi

Karatasi hii ya mambo muhimu inapeana maelezo machache tu. Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, wasiliana na:

Idara ya Kupangisha Makaazi